# MADA KUU KATIKA MAFUNZO JAMII YA KIKATOLIKI

Desturi za kikatoliki zinatufundisha ya kuwa heshima ya binadamu yaweza kulindwa na afya ya jamii yaweza kupatikana tu iwapo haki za watu zitalindwa na majukumu yao kukidhiwa. Kwa hivyo, kila mtu ana haki ya kimsingi ya kuishi vile vile kila mtu ana haki ya kupata vitu vile vinavyomwezesha kuishi maisha yenye heshima.

Sambamba na hizi haki za kibinadamu, ni majukumu na wajibu wa binadamu kwa binadamu mwenzake, majukumu na wajibu wa binadamu kwa familia na majukumu na wajibu wa binadamu kwa jamii nzima.



## UHAI WA MTU NA HESHIMA YA MTU

Kanisa katoliki linamini na linatangaza ya kwamba uhai wa mtu ni mtakatifu na heshima ya mtu ndio msingi wa maadili mema katika jamii. Imani hii ndiyo msingi wa mafunzo ya jamii ya kikatoliki. Katika jamii ya sasa, Uhai wa binadamu unapigwa vita vikali kupitia uavyaji wa mimba na ukatizaji wa maisha ya wagonjwa kwa kuwapa dawa za kuwaua haraka.
Uhai wa binadamu sasa unatishwa na technologia ya kuzalisha mapacha na kuchanganya mbegu za uzazi ili watoto watakaozaliwa wawe chaguo la mzazi/wazazi. Kwa mfano, mama anaweza kutiwa mimba kisayanzi ili azae wavulana tu au wenye akili tu na kadhalika. Kuna adhabu ya kifo kwa wanafungwa, kuna vita vinavyozushwa kimaksudi ili watu wafe na kuna mashambulizi ya kigaidi. Yote haya ni mitindo mibaya inayotishia maisha ya binadamu.

Mafunzo ya kikatoliki yanatutaka tuepukane na vita. Mataifa yetu lazima yalinde uhai, lazima yatetee haki ya binadamu kuishi. Mataifa yanaweza kutafuta njia mwafaka zinazozuia migogoro na zinazotatua ugomvi kwa njia ya Amani.


Tunaamini ya kuwa kila mwanadamu ni muhimu sana, ya kwamba watu ni muhimu kuliko vitu na ya kwamba kipimo cha ubora wa chuo chochote kile unapimwa na jinsi gani chuo hicho kinakuza au kutisha maisha na heshima ya watu wake.



## WITO KWA FAMILIA, JUMUIA NA KUSHIRIKI

Binadamu ni mtakatifu na pia ni mwana jamii. Jinsi tinavyopanga jamii zetu kiuchumi na kisiasa, kisheria na kisera inaathiri moja kwa moja heshima ya watu na uwezo wao binafsi kukua katika jamii.


Ndoa zetu na familia zetu ni vyuo muhimu katika jamii zetu, ni lazima ndoa na familia zitetewe na kuimarishwa badala ya kudhalilishwa. Tunaamini kuwa watu wana haki na wajibu wa kushriki katika maendeleo ya jamii, kutafuta pamoja mali ya umma na ustawi wa watu wote hasa watu maskini na wasiojiweza.




## HAKI NA MAJUKUMU

Desturi za kikatoliki zinatufundisha ya kuwa heshima ya binadamu yaweza kulindwa na afya ya jamii yaweza kupatikana tu iwapo haki za watu zitalindwa na majukumu yao kukidhiwa. Kwa hivyo, kila mtu ana haki ya kimsingi ya kuishi vile vile kila mtu ana haki ya kupata vitu vile vinavyomwezesha kuishi maisha yenye heshima. Sambamba na hizi haki za kibinadamu, ni majukumu na wajibu wa binadamu kwa binadamu mwenzake, majukumu na wajibu wa binadamu kwa familia na majukumu na wajibu wa binadamu kwa jamii nzima.

Tafsiri kutoka Loyola University New Orleans
http://cnh.loyno.edu/lim



## CHAGUO KWA AJILI YA MASKINI NA WASIOJIWEZA

Maadili yetu yatapimwa kwa jinsi gani watu wasiojiweza walivyo katika jamii zetu. katika jamii inayokumbwa na migawanyiko kati ya tajiri na maskini, desturi zetu zinatukumbusha hadithi ya hukumu ya mwisho (Mt. 25:31-46), pia desturi zetu zinatufundisha kuyapa kipaumbele mahitaji ya watu maskini na wasiojiweza.




## HESHIMA KWA KAZI NA HAKI ZA WAFANYAKAZI


Uchumi lazima utumikie wanadamu si vinginevyo. kazi ni Zaidi ya mapato yanayokidhi maisha, kazi ni namna ya kuendeleza ushirika wetu na Mungu katika uumbaji. Iwapo heshima ya kazi italindwa, basi haki za kimsingi za wafanyakazi lazima ziheshimiwe-

Haki ya kufanya kazi inayozaa matunda.

Haki ya kupata mshahara mzuri na wakuridhisha.

Haki ya kujiunga na vyama vya wafanyakazi.


Haki ya kumiliki mali yako binafsi na haki ya kujipanga kiuchumi.




## MSHIKAMANO

Sisi sote ni familia moja ya binadamu hata kama uraia wetu, kabila zetu, uchumi wetu na mawazo yetu ni tofauti. Tunapaswa kulindana kama ndugu na dada popote pale tulipo.

Kumpenda jirani kuna mielekeo mbalimbali katika ulimwenguni huu inaopungua. katika mada hii ya mshikamano, kuna utafutaji wa haki na Amani. Mtakatifu Papa Paul VI alifundisha kwamba, "Iwapo unataka Amani, itumikie haki." Injili inatualika tuwe watu wa Amani. Upendo wetu kwa dada na ndugu zetu unatutaka tuendeleze Amani katika dunia yetu, dunia ambayo imezingirwa na vurugu na pia migogoro.




## KULINDA VIUMBE VYA MUNGU

Tunaonyesha heshima kwa muumba wetu kwa kuvilinda na kuvitunza vema viumbe vyake. Kuilinda dunia sio tu kauli mbiu tunayotamka tunapoadhimisha siku ya dunia, Imani yetu inatuhitaji tuilinde dunia. Tunatakiwa kuwalinda watu na dunia yetu, kuishi Imani yetu kwa kuwa na mahusiano mema na viumbe vyete vya Mungu . Changamoto za kimazingira tulizonazo, zinatokana na migawanyiko ya maadili yetu. Hili sio jambo la kutupiliwa mbali. Ni swala nyeti la kuzingatiwa.

MUUNGANO WA MAASKOFU WA KANISA KATOLIKI · UNITED STATES CONFERENCE OF CATHOLIC BISHOPS

CRS CATHOLIC RELIEF SERVICES · HUDUMA ZA MISAADA ZA KANISA KATOLIKI

Mada hizi zimezalishwa na Muungano wa Maaskofu wa Kanisa Katoliki la Marekani, *Kushiriki Mafundisho Jamii ya Kikatoliki: Changamoto na Maelekezo*. Hati miliki 2017, Muungano wa Maaskofu wa Kanisa Katoliki la Marekani na Huduma za misaada za Kanisa Katoliki. Haki zote zimehifadhiwa. Picha kwa heshima ya Ndugu Mickey McGrath, OSFS..

[1] Paulo VI, *Kwa Sherehe ya Siku ya Amani* (Roma: Januari 1, 1972).